Waraka wa Sala wa Mwezi Novemba 2026

NIA ZA SALA ZA BABA MTAKATIFU

Kila mwezi, Baba Mtakatifu huukabidhi Mtandao wake wa Sala Ulimwenguni nia za sala. Nia hizi hutuelekeza kujiunga naye katika kujali utu na utume wa kanisa. Nia hizi ni wito kwa ulimwengu wote kuziweka sala zetu katika matendo mahsusi; ni dira ya utume wa huruma kwa ulimwengu.

Nia ya Sala ya Papa, Novemba 2026:

Kwa matumizi sahihi ya mali:

Tusali kuombea matumizi mazuri ya mali, kwamba tusiangukie kishawishi cha ubinafsi, bali mali daima itumike kwa manufaa ya wote na kwa usaidizi wa wale waliopungukiwa nayo.

SALA YA MWEZI NOVEMBA 2026

Kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina.

Ee Bwana wa uzima,
kila tulichonacho kinatoka kwako:
ardhi yenye rutuba, vipaji tulivyonavyo,
na juhudi za wale waliotutangulia.
Hakuna kilicho chetu peke yetu—vyote ni zawadi tuliyokirimiwa

Hata hivyo mara nyingi, Bwana, tunaruhusu mali tunayotafuta au tuliyopata
kufanya mioyo yetu kuwa migumu,
kutuweka katika gereza la ubinafsi,
na kutufanya tuwasahau maskini wahitaji.

Tusamehe kwa kulimbikiza maghalani badala ya kutoa msaada,
kwa kutumia mali kama vyombo vya mabavu badala ya huduma.

Unatukumbusha kuwa utajiri wa kweli
haupo katika vile tunavyojiwekea
bali katika tunachotoa kwa upendo.

Moyo usiofungwa na mali hubadili ulimwengu:
hufungua njia za haki,
hubomoa kuta za kutojali wengine,
na kupanda mbegu ya tumaini miongoni mwa maskini

Tunakuomba, Bwana,
Roho wako atufundishe kutumia tulivyonavyo—
pesa, muda, vipaji, fursa mbalimbali—
kama vyombo vya udugu.

Jalia kila uamuzi wa kiuchumi, kifamilia au kijumuia
uwe kutoka katika moyo ulio huru,
moyo unaotambua kwamba kila kitu kimekusudiwa kwa ajili ya wote,
na ni katika kutumia pamoja tu, ndiyo tunajenga kesho yetu.

Tufanye tuwe mashahidi wa utajiri
unaobadilishwa kuwa utumishi na huruma,
ili maisha yetu, yakiungana na maisha ya wengine,
yawe ishara ya Ufalme wako wa haki na amani.

Amina

TABIA ZA KUJIJENGEA ILI KUISHI NIA YA SALA YA MWEZI NOVEMBA 2026

1. ***Tambua kwamba kila kitu ni zawadi***
   Hakuna tulichonacho ambacho si cha kupewa. Kila siku, toa shukrani kwa kile ulichozawadiwa bila kuwa na mastahili kamili.

2. ***Toa kwa ukarimu***
   Utajiri hupimwa si kwa kile unachojilimbikizia, bali kwa kile unachotoa. Unga mkono mipango ya kusaidiana na hamasisha moyo wa kutoa kwa wahitaji.

3. ***Tumia kwa uangalifu***
   Kila ununuzi ni uamuzi wa kimaadili na wa kiroho. Jiulize: *"Je, kweli nahitaji hiki? Je, matumizi haya yanaendeleza haki au ni kwa ajili ya starehe yangu tu?"*

4. ***Fanya vipaji vyako viwe kwa huduma ya wote***
   Ujuzi wako, muda wako, na mtandao wako — hivi pia ni aina za utajiri. Vitumie kuwasaidia wale waliopungukiwa hivi ulivyonavyo.

5. ***Ishi kwa unyenyekevu wa Kiinjili***
   Unyenyekevu si kujinyima kunakoleta uchungu, bali ni uhuru wa ndani. Chagua mtindo wa maisha ulio rahisi unaojali yale yaliyo muhimu.

SALA YA MAJITOLEO YA KILA SIKU

Ee Baba mwema,
natambua uko hapa pamoja nami.
Nakuja mbele yako katika siku hii mpya.
Weka moyo wangu kwa mara nyingine tena karibu na Moyo wa Mwanao Yesu,
anayejitoa kwa ajili yangu na anayekuja kwangu katika Ekaristi.
Roho wako Mtakatifu anifanye kuwa rafiki na mtume wake,
aliye tayari kwa utume wake wa huruma ulimwenguni.

Ninaweka mikononi mwako furaha na matumaini yangu,
kazi zangu na maumivu yangu, mimi mzima na kila kitu nilichonacho,
kwa kushirikiana na kaka na dada zangu wa Mtandao huu wa Sala Ulimwenguni.

Pamoja na Mama Maria, ninakutolea siku yangu kwa ajili ya utume wa Kanisa
na kwa nia ya Sala ya Baba Mtakatifu [na Askofu wangu] kwa mwezi huu. **Amina**.